



MASWALI YANAYOULIZWA SANA (FAQs): CHANJO YA COVID-19



Ufadili unatolewa na IL Dept. of Public Health

S: Ikiwa tayari nilikuwa na COVID-19, bado ninahitaji chanjo?

J: NDIYO; kingamwili ya asili ya COVID-19 inadumu tu miezi michache na inahuza zaidi kibadala ulichoambukizwa. Kingamwili ya asili HAITAKUKINGA kwa muda mrefu na HUTAKINGWA kikamilifu dhidi ya vibadala vingine ya COVID-19.

S: Je, madhara ya chanjo ni gani?

J: Kwa watu wengi, madhara kutokana na chanjo ni kidogo na yanaweza kudumu hadi saa 36-48, ikiwemo homa, maumivu ya misuli na ya kichwa.

Mikabiliano mibaya ni nadra, lakini utachunguzwa kwa dakika 15-20 baada ya kila dozi ili kuhakikisha kuwa unahisi vizuri. Ikiwa ulikuwa na mikabiliano ya chanjo nyingine, wasiliana na daktari wako kabla ya kupata chanjo ya COVID-19.

S: Je, kuna kifaa cha ufuatiliaji katika chanjo?

J: HAPANA; chanjo zote 3 HAZITADUNGA kifaa cha ufuatiliaji kwenye mwili wako. Chanjo hazina kifaa hicho pia.

S: Je, ninapaswa kupata chanjo nikiwa mjamzito au ikiwa ninataka kupata ujauzito siku zijazo?

J: NDIYO; Chanjo HAITAKUDHURU wewe wala mtoto wako ukiwa mjamzito - isitoshe, watoa huduma wa afya na wanayasayansi wanapendekeza kwamba kina mama wajawazito wazue uwezekano wa maambukizi mabaya na madhara yanayodumu muda mrefu kwa kina mama wajawazito na watoto ambaa hawajazaliwa. Chanjo ni salama pia kwa wale wanaojaribu kupata ujauzito sasa au baadaye. Chanjo HAISABABISHI utasa/ugumba wala matatizo ya uwezo wa kubeba ujauzito.

S: Je, ninaweza kupata COVID-19 kutoka kwenye chanjo?

J: HAPANA; chanjo zote 3 HAZIWEZI kukuambukiza COVID-19. Chanjo HAZINA virusi hai. Zinachofanya tu ni kufunza seli zako jinsi ya kuunda kingamwili dhidi ya COVID-19 ili kupambana na maambukizi ukikutana na virusi.

S: Je, chanjo itaubadilisha msimbojeni (DNA) wangu?


J: HAPANA; chanjo HAITABADILISHA msimbojeni (DNA) wako kwa njia yoyote. Chanjo ina tu nyenzo za kijeni za protini ya sehemu ya juu, si virusi vyote. Haitabadilisha msimbojeni wowote katika kiini cha seli zako.

S: Je, chanjo zilitengenezwa je haraka? Ninaweza kuziamini?

J: Teknolojia iliyotumika katika chanjo hazikuundwa haraka unavyodhani. Chanjo za Pfizer na Moderna hutumia teknolojia ya mRNA, ambayo imekuwepo na imefanyiwa utafiti kwa takribani miongo 2.

Teknolojia hii imefanyiwa utafiti tangu milipuko ya SARS na MERS mapema miaka ya 2000. Chanjo ya Janssen (J&J) hutumia vekta ya virusi (si virusi hai), ambayo chanjo nyingine nyingi hutumia na mbinu hii imefanyiwa utafiti kwa miongo. Chanjo za COVID-19 ziliweza kutengenezwa haraka ili kushughulikia mgogoro wa kimataifa kutokana na utafiti wa miango minge wa jinsi ya kutumia teknolojia kwa njia salama na kwa ufanisi.

**AMINI UKWELI, PATA
CHANJO!!**



Will County
Health Department &
Community Health Center

Will County
MAPP
COLLABORATIVE

